TANGAZO LA SERIKALI Na 10 La Tarehe 3/1/2025

SHERIA YA SERIKALI ZA MITAA (MAMLAKA ZA WILAYA),
(SURA YA 287)

# SHERIA NDOGO

*(Imetengenezwa chini ya kifungu cha 153)*

SHERIA NDOGO YA UDHIBITI NA USIMAMIZI WA MIFUGO YA HALMASHAURI YA WILAYA YA MADABA YA MWAKA 2024

Jina

1. Sheria Ndogo hii itajulikana kama Sheria Ndogo ya Udhibiti na Usimamizi wa Mifugo ya Halmashauri ya Madaba ya Mwaka 2024.

Matumizi

2. Sheria Ndogo hii itatumika eneo lote la mamlaka ya Halmashauri ya Wilaya ya Madaba.

Tafsiri

3. Katika Sheria Ndogo hii, isipokuwa kama muktadha utahitaji vinginevyo-

"Afisa Mwidhiniwa" maana yake ni afisa yeyote aliyeteuliwa na Mkurugenzi kwa lengo la kusimamia utekelezaji wa Sheria Ndogo hii;

"afya" maana yake ni hali timilifu ya kimwili na kiakili ya mnyama;

"Halmashauri" maana yake ni Halmashauri ya Wilaya ya Madaba;

"kaya" maana yake ni familia ya watu akiwemo baba, mama, mtoto au watoto na mtu mwingine yeyote anayeishi na familia hiyo, au watu wanaokaa katika nyumba moja na kuishi kama familia au mtu yeyote anayeishi peke yake katika chumba au nyumba;

"kero au chukizo" maana yake ni kitu chochote ambacho kipo katika hali yoyote iwe kinatumika au kimewekwa au kimejengwa au ni kichafu kiasi cha kusababisha:

(a) hatari kwa viumbe na maisha ya binadamu;
(b) harufu mbaya ya kuudhi;

(c) kuzaliana kwa wadudu na wanyama hatari kama vile inzi, mende, sisimizi, panya, nyoka, nyuki, kunguni au viumbe wengine hatari;

(d) magonjwa kwa binadamu, kuhifadhi mbu, inzi, panya na viumbe wenye madhara;

"kibali" maana yake ni idhini ya maandishi inayotolewa na Halmashauri kwa ajili ya kufanya shughuli iliyokusudiwa chini ya Sheria Ndogo hii;

"machinjio" maana yake ni sehemu iliyotengwa na Halmashauri kwa ajili ya kuchinjia wanyama na kuanika ngozi ikiwa ni pamoja na maeneo ya taasisi ya umma au watu binafsi yaliyopo katika eneo la Halmashauri;

"meneja wa machinjio" maana yake ni Meneja wa Machinjio yanayomilikiwa na Halmashauri aliyeteuliwa kwa mujibu wa Hati ya Uanzishaji wa Bodi ya Huduma ya Machinjio ya Halmashauri;

"mifugo" maana yake ni ng'ombe, mbuzi, kondoo, kuku au wanyama wengine wanaofugwa na binadamu;

"mkaguzi wa nyama" maana yake ni mtaalam wa afya ya mifugo aliyeajiriwa na Serikali na kusajiliwa, kuorodheshwa au kuandikishwa na Baraza la Veterinari Tanzania;

"Mkurugenzi" maana yake ni Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Madaba au afisa yeyote atakayeteuliwa kutekeleza majukumu ya Mkurugenzi;

"mmiliki wa machinjio" maana yake ni mtu yeyote anayemiliki machinjio binafsi katika eneo la Halmashauri;

"Wakala" maana yake ni mtu binafsi, kikundi, taasisi, shirika au kampuni iliyoteuliwa kwa ajili ya kusimamia utekelezaji wa Sheria Ndogo hii kwa niaba ya Halmashauri.

Wajibu wa Halmashauri

4. Halmashauri itakuwa na wajibu wa kufanya mambo yafuatayo:

(a) kuandaa mpango wa matumizi bora ya ardhi;

(b) kuelekeza idadi ya mifugo ambayo kila mfugaji anaruhusiwa kufuga kulingana na ukubwa wa eneo lake;
(c) kujenga majosho ya mifugo kwa kushirikiana na wananchi;
(d) kutoa elimu ya ufugaji bora kwa jamii ili kuongeza tija;
(e) kufanya sensa ya mifugo, kuweka alama na kutoa kadi za mifugo;
(f) kutoa chanjo kwa kushirikiana na wafugaji ili kudhibiti magonjwa ya mifugo yasiyoambukiza na yanayoambukiza binadamu; na
(g) kudhibiti uzururaji holela wa mifugo na wanyama katika Halmashauri kwa mujibu wa sheria.

Wajibu wa mfugaji

5. Kila mfugaji katika eneo la Halmashauri atahakikisha kuwa:
(a) anaogesha mifugo yake ili kudhibiti magonjwa ya wanyama kama atakavyoelekezwa na Halmashauri;
(b) mifugo yake inawekwa alama maalumu zinazotolewa kwa mujibu wa Sheria ya Ustawi wa Wanyama; Sura ya 154
(c) anahudhuria mafunzo ya ufugaji kama atakavyohitajika na Halmashauri;
(d) anafuga idadi ya mifugo katika jengo lililoidhinishwa kulingana na maelekezo yaliyoainishwa katika Jedwali la Kwanza;
(e) anakuwa na kadi ya mifugo itakayoonesha idadi na aina ya mifugo aliyonayo;
(f) anaipatia mifugo yake malisho au chakula na maji ya kutosha kwa kuzingatia kanuni bora za ufugaji;
(g) anafuga kwa kuzingatia mipango ya matumizi bora ya ardhi;
(h) anapeleka mifugo yake katika vituo vya chanjo kama itakavyoamriwa na Halmashauri na atalipia chanjo hiyo kama atatakiwa kufanya hivyo kwa mujibu wa viwango vitakavyoainishwa na mamlaka husika; na

(i) anauza mifugo yake katika masoko na minada iliyoidhinishwa au eneo lingine kwa taarifa maalum.

Kibali cha kufuga wanyama

6.-(1) Mtu yeyote anayekusudia kufuga mifugo atapaswa kupata kibali cha kufuga kutoka kwa Halmashauri kama ilivyoainishwa katika Jedwali la Pili.

(2) Kibali cha ufugaji kitatolewa bure na kitakuwa cha miaka mitatu kuanzia tarehe kilipotolewa.

(3) Bila kuathiri kanuni ndogo ya (1) na (2), endapo mtu yeyote atakiuka taratibu za ufugaji zilizoelekezwa chini ya Sheria Ndogo hii, Halmashauri itafuta kibali cha ufugaji cha mtu huyo na atalazimika kuhamisha mifugo yake yote kutoka katika eneo la Halmashauri.

Masharti kwa mfugaji

7. Kila mfugaji hataruhusiwa:

(a) kuchunga, kulisha au kunywesha maji mifugo katika maeneo ambayo hayakutengwa kwa shughuli hiyo;
(b) kusafirisha mifugo kwa kuiswaga barabarani;
(c) kusafirisha au kuhamisha mifugo kutoka eneo moja hadi lingine bila kibali kutoka Halmashauri;
(d) kuingiza mifugo katika eneo la Halmashauri bila kibali;
(e) bila kibali maalum cha Halmashauri, kuuza au kununua mifugo katika maeneo ambayo siyo mnada, masoko au magulio ya mifugo yaliyoidhinishwa; na
(f) kununua, kuuza au kufanya biashara ya kubadilishana aina yoyote ya mifugo katika eneo la Halmashauri bila kibali maalum isipokuwa kwenye minada au magulio yaliyotengwa kwa shughuli hiyo na Halmashauri.

Kibali cha kusafirisha mifugo

8.- (1) Mtu yeyote anayekusudia kusafirisha mifugo au mazao ya mifugo kutoka au kuingia katika eneo la Halmashauri atatakiwa kuwa na kibali maalumu kama ilivyoainishwa katika Jedwali la Tatu.

(2) Halmashauri itatoa kibali cha kusafirisha mifugo kwa kuweka utaratibu ikiwa ni pamoja na:

(a) mfugaji kutoa uthibitisho wa kumiliki mifugo kwa kujaza fomu maalumu ilivyoainishwa katika Jedwali la Nne; na

(b) kukagua kibali cha kusafirisha mifugo.

(3) Afisa Mwidhiniwa atakuwa na uwezo wa kukamata na kutoza faini na adhabu kwa mifugo yoyote inayosafirishwa kinyume na Sheria Ndogo hii.

(4) Muda wa kusafirisha mifugo na mazao ya mifugo kutoka Halmashauri itakuwa ni kuanzia saa kumi na mbili kamili alfajiri hadi saa kumi na mbili kamili jioni.

Kudhibiti mifugo inayozurura ovyo

9.-(1) Halmashauri itakamata mifugo yoyote itakayoonekana inazurura ovyo katika eneo la Halmashauri.

(2) Mmiliki wa mifugo itakayokamatwa chini ya kanuni ndogo ya (1) atalipa faini ya kiasi cha shilingi elfu kumi kwa kila siku.

(3) Endapo mifugo iliyokamatwa haitachukuliwa na mmiliki ndani ya kipindi cha siku saba tangu kukamatwa, Halmashauri itakuwa na haki ya kuuza kwa mnada mifugo hiyo baada ya kupata idhini ya Mahakama, na fedha zitakazopatikana zitarejeshwa kwa mmiliki wa mifugo baada ya kutoa faini inayodaiwa, gharama za kuhifadhi mifugo, gharama ya mahakama na gharama ya mnada.

(4) Bila kuathiri kanuni ndogo ya (3), kabla ya Halmashauri kuuza kwa mnada mifugo iliyokamatwa, Mkurugenzi atamjulisha mmliki na umma juu ya kusudio hilo.

(5) Endapo kutatokea kufa kwa mifugo kutokana na sababu yoyote, Halmashauri haitawajibika na ulipaji wa gharama zozote isipokuwa kama vifo hivyo vitakuwa vimesababishwa na uzembe wa watumishi wa Halmashauri.

Ukaguzi wa mifugo na bidhaa za mifugo

10.-(1) Afisa Mwidhiniwa atakuwa na uwezo wa kukataa aina yoyote ya mifugo au bidhaa kuingia au kuuzwa ndani ya eneo la Halmashauri, iwapo mifugo hiyo au bidhaa hizo zinaweza kuhatarisha afya au usalama wa mifugo mingine au watumiaji.

(2) Afisa Mwidhiniwa anaweza kuingia katika nyumba au jengo lolote kuanzia saa kumi na mbili asubuhi hadi saa kumi na mbili jioni kwa lengo la utekelezaji wa Sheria Ndogo hii.

Taratibu za biashara ya mifugo na mazao ya mifugo

11.-(1) Kabla ya kuanza biashara ya mifugo au mazao ya mifugo, mfanyabiashara atapaswa kuwa na leseni, utambulisho na vibali kutoka mamlaka husika vinavyohusu kuuza na kununua mifugo au mazao ya mifugo na atatakiwa kuwasilisha vibali vyake Halmashauri kwa ajili ya uhakiki.

(2) Mfanyabiashara atakayesafirisha mifugo kutoka nje ya Halmashauri atatakiwa kuwa na kibali kutoka Halmashauiri ambayo mifugo hiyo inatoka.

(3) Bila kuathiri masharti ya kanuni ndogo ya (2), mfanyabiashara wa mifugo atatakiwa kusafirisha mifugo katika vyombo vya usafiri vinavyokubalika kwa mujibu wa sheria.

(4) Mifugo yote itauzwa au kununuliwa katika minada na masoko yanayotambulika kwa mujibu wa sheria.

Wajibu wa mfanyabiashara wa bucha na maduka ya nyama

12. Kila mfanyabiashara wa bucha au duka la nyama anatakiwa kuhakikisha kuwa:

(a) ana leseni na vibali vya kufanya biashara hiyo;
(b) kuna kabati la vioo la kuzuia nzi na wadudu wengine wataambao;
(c) kuna pipa la kuhifadhia taka ngumu na laini;
(d) kuna jokofu la kuhifadhia nyama;
(e) jengo lake la biashara lina mwanga wa kutosha, umeme, maji safi na salama, visu, meza, mzani wa kawaida au mzani wa kielektroniki na misumeno maalumu ya kukatia nyama;
(f) nyama imekaguliwa na mkaguzi aliyeidhinishwa na imegongwa muhuri na inauzwa ndani ya jengo;
(g) muuzaji anavaa sare nyeupe muda wote inayojumuisha mabuti, koti na kofia;

(h) muuzaji anapima afya yake kila baada ya miezi sita na kuhakikisha anakuwa na cheti cha upimaji;

(i) mmiliki wa bucha au muuzaji wa nyama anatoa ushirikiano wa kutosha kwa wakaguzi mara atakapotakiwa kufanya hivyo wakati wowote wa ukaguzi; na

(j) biashara ya nyama inafanyika katika bucha au duka maalumu na sio vinginevyo.

Usafirishaji wa Nyama

13.-(1) Mfanyabiashara wa nyama atatakiwa kusafirisha nyama kutoka machinjioni kwa kutumia gari maalumu na endapo atatumia usafiri wa pikipiki au baiskeli atatakiwa kubeba nyama kwa kutumia chombo maalumu kilichoidhinishwa na Halmashauri.

(2) Kila mmiliki wa gari la kubeba nyama atahakikisha kuwa gari lake:

(a) limesajiliwa na kupewa cheti maalumu cha ukaguzi na Halmashauri;

(b) linakaguliwa kila baada ya miezi mitatu;

(c) lina sanduku la aluminiamu lenye mfuniko na limepakwa rangi nyeupe, mstari mwekundu na namba; na

(d) halibebi kitu kingine tofauti na nyama.

(3) Mmiliki wa gari la kubeba nyama atapaswa kulipia gharama za usafirishaji kama zitakavyowekwa na Halmashauri.

Kuingiza wanyama katika machinjio

14.-(1) Meneja wa machinjio au mmiliki wa machinjio atakuwa na wajibu wa kuhakikisha kuwa umiliki wa mnyama anayekusudiwa kuchinjwa unathibitishwa kabla ya kuingizwa katika eneo la machinjio.

(2) Bila kuathiri kanuni ndogo ya (1), meneja wa machinjio au mmiliki wa machinjio atawajibika kukagua kibali cha usafirishaji wa mnyama na nyaraka nyingine zinazothibitisha umiliki.

(3) Meneja wa machinjio au mmiliki wa machinjio atatunza rejista ya wanyama waliopokelewa machinjioni ambayo itaainisha aina ya mnyama, jinsi, umri na taarifa za mmiliki.

Ukaguzi wa wanyama

15.-(1) Mnyama yeyote anayekusudiwa kuchinjwa katika machinjio atafanyiwa ukaguzi wa awali na Mkaguzi wa Nyama kabla ya kuchinjwa.

(2) Mnyama ambaye baada ya ukaguzi atagundulika kuwa na ugonjwa unaohatarisha afya ya binadamu atahifadhiwa katika eneo maalum la kuhifadhi wanyama wenye magonjwa kwa ajili ya matibabu.

Sura ya 156

(3) Kabla ya mnyama kutengwa, taratibu zilizoainishwa katika Sheria ya Magonjwa ya Wanyama zitafuatwa.

(4) Endapo mnyama aliyetengwa kwa mujibu wa kanuni ndogo ya (2) ataendelea kuwa na ugonjwa uliosababisha atengwe, Afisa Mwidhiniwa atamtaka mmiliki wa mnyama huyo kumtoa nje ya eneo la machinjio kwa matibabu zaidi.

(5) Endapo mmiliki atashindwa kumwondoa mnyama aliyetengwa ndani ya muda wa saa kumi na mbili tangu amri ya kuondolewa kwa mnyama itolewe, Afisa Mwidhiniwa anaweza kuamuru mnyama huyo kuteketezwa kwa gharama ya mmiliki.

(6) Afisa Mwidhiniwa atakuwa na wajibu wa kuchukua taarifa za mmiliki na kumbukumbu za mnyama aliyebainika kuwa na ugonjwa na kumweka alama maalum itakayomtambulisha mnyama huyo.

Udhibiti wa uchinjaji machinjioni

16.-(1) Watu wote wanaohusika na shughuli za machinjio, watatakiwa kupima afya kila baada ya miezi sita.

(2) Watu wanaohusika na machinjio wanatakiwa kuwa wasafi na kuvaa mavazi maalumu kwa ajili ya kazi hiyo.

(3) Mtu yeyote hataruhusiwa kukaa au kufanya mkusanyiko wa aina yoyote katika eneo la machinjio isipokuwa kwa kibali maalumu kitakachotolewa na Halmashauri.

(4) Meneja au mmiliki wa machinjio atahakikisha kuwa shughuli za uendeshaji wa machinjio zinazingatia sheria na taratibu za afya.

(5) Mtu hataruhusiwa kufanya biashara ya aina yoyote katika eneo la machinjio.

(6) Mtu hataruhusiwa kuweka bucha, duka la nyama au biashara yoyote ya nyama ndani ya mita 200 kutoka eneo la machinjio.

(7) Mfanyabiashara wa nyama atapaswa kuwa na utambulisho kutoka Bodi ya Nyama na leseni halali ya biashara.

(8) Kila mfugaji atatakiwa kupeleka mifugo yake machinjioni au mahali huduma hiyo inapopatikana na itakuwa ni marufuku kwa mtu yeyote kuchinja mifugo mahali pengine popote ambapo sio machinjio isipokuwa kwa kutoa taarifa kwa Afisa Mwidhiniwa na mfugaji atalazimika kulipia gharama za machinjio kwa kuzingatia viwango vilivyoainishwa katika Sheria Ndogo hii.

(9) Nyama yoyote haitaruhusiwa kutumika kwa matumizi ya binadamu bila kufanyiwa ukaguzi wa mwisho na kuwa na muhuri maalumu wa ukaguzi nyama.

(10) Mtu yeyote hataruhusiwa kuingiza mifugo katika machinjio kwa ajili ya kuchinja baada ya saa kumi na moja kamili jioni isipokuwa kwa kibali maalumu cha Halmashauri.

(11) Mtu yeyote hataruhusiwa kutoa nje ya eneo la machinjio mnyama aliye hai au aliyekufa au nyama bila ya idhini ya maandishi ya meneja wa machinjio au mmiliki wa machinjio.

(12) Meneja wa machinjio au mmiliki wa machinjio hataruhusu mifugo yoyote kuchinjwa bila kufanyiwa ukaguzi wa awali.

(13) Mtu yeyote hataruhusiwa kutoa lugha za kashfa, kuudhi, kudhalilisha au matusi kwa mtaalamu au mtu yeyote katika eneo la machinjio.

Ukaguzi wa nyama

17.-(1) Mkaguzi wa Nyama atakuwa na wajibu wa kukagua nyama katika eneo la machinjio baada ya mnyama kuchinjwa kwa madhumuni ya kubaini iwapo nyama inafaa kwa matumizi ya binadamu.

(2) Endapo itabainika kuwa nyama iliyokaguliwa:

(a) inafaa kwa matumizi ya binadamu, Mkaguzi wa Nyama atagonga nyama hiyo muhuri

unaothibitisha kuwa nyama iliyokaguliwa ni salama kwa matumizi ya binadamu; au

(b) haifai kwa matumizi ya binadamu, nyama hiyo itateketezwa kwa kuichoma moto au kwa njia nyingine itakayoonekana inafaa na Afisa Mwidhiniwa atachukua kumbukumbu za nyama hiyo na za mmiliki wake.

(3) Endapo matokeo ya vipimo vya awali yatakuwa na mashaka kuhusu usalama wa nyama kwa matumizi ya binadamu, Mkaguzi wa Nyama atahakikisha kuwa nyama husika inahifadhiwa kwa muda usiozidi saa ishirini na nne ili kuruhusu vipimo zaidi vya kimaabara kufanyika.

(4) Meneja wa machinjio au mmiliki wa machinjio atatunza rejesta ya nyama zilizokaguliwa ambayo itaonesha aina ya nyama, jinsi, umri, uzito na taarifa za mmiliki na kama nyama inafaa au haifai kwa matumizi ya binadamu.

Udhibiti wa ufugaji wa mbwa

18.-(1) Mtu yeyote hataruhusiwa kufuga mbwa katika eneo la Halmashauri bila kibali cha ufugaji kutoka Halmashauri.

(2) Kibali cha ufugaji kitatolewa bure na kitadumu kwa muda wa mwaka mmoja.

(3) Mfugaji atawajibika kumpatia chanjo mbwa wake na kulipa ada ya chanjo kama atakavyoelekezwa na Halmashauri.

(4) Mfugaji atalazimika kuonesha cheti cha chanjo ya mbwa kabla ya kupata au kuhuisha kibali kilichoisha muda wake.

(5) Mfugaji atawajibika kumfungia mbwa wake wakati wote wa mchana na anaweza kumfungulia kuanzia saa nne kamili usiku na kumfungia saa kumi na moja alfajiri.

(6) Mfugaji atawajibika kuogesha mbwa kila baada ya siku saba ili kudhibiti magonjwa na wadudu wasumbufu kwa gharama zake na kama atakavyoelekezwa na Halmashauri.

(7) Mfugaji atalazimika kumfunga mbwa kwa mnyororo maalumu wakati wa kutembea nae kutoka sehemu moja kwenda sehemu nyingine.

(8) Iwapo mfugaji anasafirisha mbwa, atalazimika kuwa na kasha maalumu kama atakavyoelekezwa na Afisa wa Mwidhiniwa la kusafirishia mbwa kabla ya kupewa kibali.

Mbwa anaezurura

19. Halmashauri inaweza kukamata na kuhifadhi katika kizuizi kwa muda usiozidi siku mbili mbwa atakayepatikana anazurura, na baada ya hapo, Halmashauri inaweza kutaifisha au kuchukua hatua nyingine kisheria kwa kadri itakavyoona inafaa.

Makosa

20. Mfugaji yeyote atakuwa ametenda kosa iwapo:

(a) atashindwa au kukataa kuogesha au kuchanja mifugo yake ili kuzuia magonjwa;

(b) atalisha mifugo kwenye maeneo yasiyoruhusiwa;

(c) kuanzisha duka la kuuza vyakula vya mifugo, ghala la kuhifadhia mifugo, kiwanda cha kutengeneza vyakula vya mifugo, vituo vya huduma za mifugo au zahanati na vituo vya kutotolesha vifaranga bila kuwa na kibali kutoka Halmashauri;

(d) atafuga mifugo katika eneo la Halmashauri bila kuwa na kibali cha ufugaji;

(e) atashindwa au atazembea kutoa taarifa kuhusu uwepo wa au dalili za ugonjwa au kifo cha ghafla katika mifugo yake;

(f) atashindwa kuwasilisha taarifa ya mwezi ya uuzaji wa vyakula vya mifugo, utengenezaji wa vyakula vya mifugo au ghala, vituo vya huduma za mifugo au zahanati na vituo vya kutotolesha vifaranga kwa afisa mwidhiniwa;

(g) atauza na kufuga mifugo pembezoni mwa barabara au sehemu ambayo haijaruhusiwa;

(h) atasababisha kero ya harufu mbaya na kelele ya mifugo yake kwa jamii;

(i) ataruhusu mifugo yake kuzurura ovyo;

(j) ataweka vyakula vya mifugo wazi;

(k) atashindwa kutoa ushirikiano wa uwekaji wa alama kwa mifugo yake;

(l) atatumia au kuingiza kilevi chochote kisichoruhusiwa katika eneo la machinjio;
(m) atatumia lugha inayoudhi ndani ya machinjio au kufanya udhalilishaji wa aina yoyote;
(n) atabandika au kubandua tangazo bila idhini ya meneja wa machinjio au mmiliki wa machinjio;
(o) atahatarisha amani au kushiriki kwa namna yeyote kuhatarisha amani katika eneo la machinjio;
(p) atafanya au kushiriki kufanya uchafuzi wa mazingira;
(q) atafanya shughuli za kisiasa ikiwa ni pamoja na kupandisha bendera ya chama cha siasa; au
(r) atamzuia afisa mwidhiniwa kutekeleza majukumu yake.

Adhabu

21. Mtu yeyote atakayepatikana na hatia kwa kutenda kosa chini ya Sheria Ndogo hii atawajibika kwa faini ya kiasi kisichopungua shilingi elfu hamsini na kisichozidi shilingi laki tatu au kifungo kisichozidi miezi kumi na mbili jela au adhabu zote mbili kwa pamoja.

Kufifilisha kosa

22. Mkurugenzi anaweza kumtoza faini mtu yeyote aliyetenda kosa chini ya Sheria Ndogo hii, kiasi cha shilingi elfu hamsini iwapo mkosaji atakiri kosa kwa hiari na kuwa tayari kujaza fomu maalumu iliyoambatanishwa kwenye Jedwali la Tano.

## JEDWALI LA KWANZA

*(Limetengenezwa chini ya kifungu cha 5(d))*

### IDADI YA MIFUGO ILIYORUHUSIWA KUFUGWA

| Namba | Aina ya Mfugo | Idadi | Maelezo |
|---|---|---|---|
| 1. | Ng’ombe | - | Mfugaji atapewa kibali cha kufuga kulingana na ukubwa wa eneo alilonalo bila kusababisha kero ya harufu na kelele kwa jamii |

*Tangazo la Serikali Na.10 (Linaendelea.)*

| | | | |
|---|---|---|---|
| 2. | Mbuzi au Kondoo | - | Mfugaji atapewa kibali cha kufuga kulingana na ukubwa wa eneo alilonalo bila kusababisha kero ya harufu na kelele kwa jamii |
| 3. | Nguruwe | 4 | Nguruwe Watoto wakiachishwa kunyonya wauzwe au kuondolewa |
| 4. | Mbwa | - | Mfugaji atapewa kibali cha kufuga kulingana na ukubwa wa eneo alilonalo bila kusababisha kero ya harufu na kelele kwa jamii |
| 5. | Wanyama wa jamii ya ndege | - | Mfugaji atapewa kibali cha kufuga kulingana na ukubwa wa eneo alilonalo bila kusababisha kero ya harufu na kelele kwa jamii |

JEDWALI LA PILI

*(Limetengenezwa chini ya kanuni ya 6(1)*

KIBALI CHA UFUGAJI

Jina la Mfugaji:………………………………………………………..
Anuani:…………………………………………………………
Kata:…………………………………… Mtaa …………………
Namba Nyumba:…………………………………… Namba Kitalu:……………
Ameruhusiwa kufuga Mifugo ifuatao katika eneo la…………..

| Na | Aina ya Mfugo | Koo | Idadi ya Mifugo | | Jumla |
|---|---|---|---|---|---|
| | | | Jike | Dume | |
| 1 | Ng'ombe | | | | |
| 2 | Mbuzi | | | | |
| 3 | Kondoo | | | | |
| 4 | Nguruwe | | | | |
| 5 | Ngamia | | | | |
| 6 | Punda | | | | |
| 7 | Paka | | | | |
| 8 | Farasi | | | | |
| 9 | Sungura | | | | |
| 10 | Mbwa | | | | |
| 11 | Kuku au Bata | | | | |
| 12 | Wanyama wengine | | | | |

Kibali hiki kimetolewa kwa Ndugu:……………………………………kwa muda wa miezi ………………….kwa Mifugo kuanzia tarehe……………..hadi tarehe…………..

Kimetolewa na:
Jina la Afisa Mwidhiniwa…………………………………….
Tarehe……………………………….
Muhuri:

JEDWALI LA TATU

*(Limetengenezwa chini ya kanuni ya 8 (1))*

KIBALI CHA KUSAFIRISHA MIFUGO

Jina:…………………………………………….
Anuani:…………………………………………
Ameruhusiwa kusafirisha Mifugo ifuatayo kutoka ………………kupitia njia za……………………..hadi…………..…..

| Namba | Aina ya Mfugo | Idadi ya Mifugo |
|---|---|---|
| 1. | Ng'ombe | |
| 2. | Mbuzi | |
| 3. | Kondoo | |
| 4. | Nguruwe | |
| 5. | Ngamia | |
| 6. | Punda | |
| 7. | Paka | |
| 8. | Farasi | |
| 9. | Sungura | |
| 10. | Mbwa | |
| 11. | Kuku au Bata | |
| 12. | Mifugo wengine | |

Kibali hiki kitakuwa cha muda wa siku….. kuanzia tarehe…....hadi tarehe……….

Kimetolewa na :
Jina la Afisa Mwidhiniwa:……………………………………….
Saini:…………………………………………………………..
Wadhifa:…………………………………………………………..
Tarehe:………………………………………………………....
Muhuri:………………………………………

JEDWALI LA NNE

*(Limetengenezwa chini ya kanuni ya 8(2)(a))*

KIBALI CHA MFUGAJI CHA KUTHIBITISHA UHALALI WA KUMILIKI MIFUGO ANAYOTAKA KUSAFIRISHA KWENDA MNADANI/KUHAMIA ENEO LINGINE

A. Jina la Mfugaji/Mmiliki: …………..………………Jina la msafirishaji…………………………
Mahusiano ya msafirishaji na Mmiliki………………………………………….

B. Anuani…………Kijiji cha………………Kitongoji cha…………… Ranchi ya…………………. Kitalu Namba………..……..

Ameruhusiwa kusafirisha wanyama wake wafuatao kwenda Mnada wa/Kijiji cha…………… kutoka ……………… kupitia njia za………………hadi…………………

| Na | Aina ya mnyama | Idadi |
|---|---|---|
| 1 | Ng'ombe | |
| 2 | Mbuzi | |
| 3 | Kondoo | |
| 4 | Nguruwe | |
| 5 | Ngamia | |
| 6 | Punda | |
| 7 | Paka | |
| 8 | Farasi | |
| 9 | Sungura | |
| 10 | Mbwa | |
| 11 | Kuku /Bata | |
| 12 | Wanyama wengine (wataje) | |

Kwa muda wote wa saa za mchana kwa kipindi cha kuanzia ………….. hadi ……….. Namba ya gari……………. Namba ya trela………….. Kibali hiki kitakuwa cha muda wa siku……….. kuanzia tarehe ………….. hadi tarehe …………..

Barua toka kwa Afisa Mtendaji /Afisa Mifugo Kijiji/Kata inayothibitisha uhalali wa kumiliki mifugo /wanyama hao imeambatanishwa.

Kimetolewa na :

Jina la Afisa Mwidhiniwa : ……………………………… Cheo …………………….

Tarehe : ………………………………….

Muhuri na Saini:

*Tangazo la Serikali Na.10 (Linaendelea.)*

*NB: KIBALI HIKI AMBACHO ATAPWEWA MWENYE MIFUGO NI MAHSUSI KWA AJILI YA KUTHIBITISHA UHALALI WA MIFUGO INAYOPELEKWA MNADANI KUUZWA/KUHAMIA ENEO LINGINE*

JEDWALI LA TANO

*(Limetengenezwa chini ya kanuni ya 22)*

FOMU YA KUKIRI NA KUFIFILISHA KOSA

Mimi …………………………………………………… nakiri KWA HIARI YANGU MWENYEWE mbele ya ………………………………………. ambaye ni Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Madaba, kwamba mnamo tarehe …… ya Mwezi ………. Mwaka ……….…… nilitenda kosa la kukiuka masharti ya kanuni ya …… ya Sheria Ndogo ya Udhibiti na Usimamizi wa Mifugo ya Halmashauri ya Wilaya ya Madaba ya Mwaka 2024.

Kwa mamlaka aliyopewa Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Madaba, niko tayari kulipa kiasi cha ada ninayodaiwa kwa kiasi cha shilingi ……………….. pamoja na faini ya kufifilisha kosa ya kiasi cha shilingi ………………………...

NATHIBITISHA KWAMBA MAELEZO HAPO JUU NI YA KWELI NA NIMEYATOA MIMI MWENYEWE KWA HIARI YANGU KADRI YA UFAHAMU WANGU

Leo tarehe…………. ya Mwezi…………..… Mwaka …………….
Jina……………………………….. Saini………………………

MBELE YANGU:
Jina:…………………………………..…………………….....
Saini……………………….…………………………..………
Wadhifa:………………………………………………………
Tarehe…………………………………………………………

*Tangazo la Serikali Na.10 (Linaendelea.)*

Lakiri ya Halmashauri ya Wilaya ya Madaba imegongwa katika Sheria Ndogo hizi kufuatia Azimio la Mkutano wa Baraza la Madiwani ulioketi katika ukumbi wa Halmashauri ya wilaya ya Madaba tarehe 28/7/2023 na kushuhudiwa lakiri hiyo ikigongwa mbele ya:-

SAJIDU IDRISA MOHAMED,
*Mkurugenzi mtendaji,*
*Halmashauri ya Wilaya,*
*Madaba*

TEOFANES TADEI MLELWA,
*Mwenyekiti,*
*Halmashauri ya wilaya,*
*Madaba*

**L.S**

**NAKUBALI**,

Dodoma,
30 Januari, 2024.

MOHAMED OMARY MCHENGERWA,
*Waziri wa Nchi OR-Tamisemi*